

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Enyi Maulamaa Waheshimiwa wa Pakistan! Gaza Inaungua, Huku Watawala wa Pakistan waki ni Watazamaji Wasiochukua Hatua. Lazima Muwanusuru Waislamu wa Gaza, kwa Kutoa Wito wa Jihad kwa Wanajeshi wa Pakistan kwa ajili ya Ukombozi wa Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina**

**(Imetafsiriwa)**

**Maulamaa waheshimiwa wa Pakistan!** Umbile la Kiyahudi linaijaza anga ya Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina moto na moshi, huku ikinywesheza ardhi yake kwa damu na machozi ya Waislamu. Miezi miwili imepita, ilhali, hakuna jeshi hata moja la Waislamu lililotaharaki kulifukuza jeshi la adui linaloshambulia. Hivyo, tunakuhutubieni kama Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) wanavyotufahamisha lazima uwe. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

[إِنَّمَا يَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ]

**“Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni.”** [Surah Fatir: 28]. Kutoka kwa Abu Ad-Dardaa’ (ra), Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema, العلماء ورثة الانبياء **“Maulamaa ni warithi wa Mitume.”** [Abu Dawud, Tirmidhi] Hivyo, baada ya zama za Mtume wa mwisho (saw) kutumwa kwa wanadamu, na mwisho wa Wahyi, ni lazima muwe kama walivyokuwa Mitume (as), kuchunga mambo ya watu, kwa yale yote aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu (swt).

**Enyi Warithi wa Mitume (as)!** Nyuma ya matukio ya mgogoro wa sasa huko Gaza, vibaraka wa Biden wanataka uungaji mkono wenu katika kuisalimisha Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina kwa umbile linaloikalia kwa mabavu la Mayahudi, kupitia “suluhisho” la Magharibi linalopigiwa debe na watawala wa Waislamu, juu ya Waarabu na Ajami (wasio Waarabu). Wanakuleteeni “suluhisho la dola mbili” kama suluhisho la hali ya sasa, ingawa hilo linaloitwa suluhisho ni udanganyifu tu. “Suluhisho la dola mbili” husababisha kuimarishwa kwa umbile la Mayahudi. Njia za kuishi kwa Waislamu nchini Palestina zitakuwa kwenye rehema ya umbile katili na lisilo na huruma la Mayahudi. Ulinzi wao utakuwa mikononi mwa umbile la Mayahudi. Zaidi ya hayo, “usuluhisho wa dola mbili” linachochea ujasiri wa umbile la Mayahudi kueneza moto wa Fitnah yake, kutoka kuwa ndani ya eneo pekee, hadi nje yake.

“Suluhisho” la Kimagharibi ni suluhisho la Marekani. Kuunga mkono “suluhisho la dola mbili” ni khiyana kwa Mwenyezi Mungu (swt), Mtume wake (saw) na waumini. Ardhi ya Waislamu ni utakatifu ambao haujuzu kwa Waislamu kuisalimisha. Mwenyezi Mungu (swt) ameharamisha kukubali aina yoyote ya utukufu wa makafiri juu ya Waislamu. Amesema Mwenyezi Mungu (swt),

[وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا]

**“wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini.”** [Surah An-Nisaa 4:141]. Mwenyezi Mungu (swt) ameifanya kuwa faradhi ya Shariah kumaliza unyakuzi wa makafiri wa ardhi za Waislamu. Amesema Mwenyezi Mungu (swt),

[وَأَخْرَجُوهُمْ مِنْ حَيْثُ أَخْرَجُوهُمْ]

**“na muwatoe popote walipo kutoeni.”** [Surah Al-Baqarah 2:191]. Amri ya Mwenyezi Mungu (swt) inahusiana na ardhi yoyote ya Waislamu, huku ardhi ya Palestina ni ardhi ya Msikiti wa Al-Aqsa, Kibla cha Kwanza, Haram iliyotakaswa, eneo la Isra'a na Miraj ya Mtume (saw), ambaye Mwenyezi Mungu (swt) amevibariki viunga vyake mpaka Siku ya Kiyama!

**Enyi Maulamaa Waheshimiwa!** Watawala wa Pakistan wanaelekea katika kulitambua umbile la Mayahudi, kwa badali ya fedha kutoka kwa watawala wasaliti wa dola za Ghuba, vibaraka wa Magharibi. Wanataka muidhinishe “suluhisho la dola mbili” la Marekani. Kwa hiyo watawala hawa wanatumia hadhi yenu ya kidini ndani ya Ummah kuimarisha misimamo yao ya khiyana. Kwa njia ya kuwaonya dhidi ya udanganyifu wa watawala hawa, tunakukumbusheni kauli ya Umar al-Farooq (ra), kama ilivyosimuliwa na ad-Darami:

هَلْ تَعْرِفُ مَا يَهْدِمُ الْإِسْلَامَ؟ قَالَ قُلْتُ، لَا. قَالَ يَهْدِمُهُ زَلَّةُ الْعَالِمِ وَجِدَالُ الْمُنَافِقِ بِالْكِتَابِ وَحُكْمُ الْأَيْمَةِ الْمُضَيَّبِينَ

**“Je, unajua ni kitu gani chenye kuvunja Uislamu?” Asema nikasema, “Hapana.” Umar akasema, “Unavunjwa kwa mtelemu wa mwanachuoni (‘Alim), na mjadala wa wanafiki juu ya Kitabu, na utoaji hukmu wa maimamu waliopotoka.”**

